BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 14 Juni, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

238. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Ni kweli kwamba ardhi ni mali ya Serikali kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar. Pamoja na Serikali kumiliki ardhi lakini imetoa haki kwa kila mtu kufanya shughuli zake pamoja na kutumia ardhi hiyo bila ya ubaguzi wa aina yoyote, kama ilivyokusudiwa na uongozi wa Awamu ya Kwanza baada ya Mapinduzi yaliyoongozwa na marehemu Mzee Abeid Karume, kwa kugawa eka tatu kwa kila Mzanzibari.

(a) Kwa nini Serikali katika awamu hii imezichukua ardhi za wakulima na wakwezi walizolelewa pamoja na kuishi na wazee wao huku wakifanya shughuli za kilimo na ufugaji katika maeneo ya Makaani Vitongoji na hatimae kuwapa wawekezaji wa ‘Crushers’.

(b) Je, kwa kiasi gani kitendo hicho kinakwenda kinyume na malengo pamoja na dhamira nzuri ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi</u>:**

201. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Malalamiko ya wananchi kwa Serikali yao kuhusiana na suala la kuwaondoa katika maeneo yao ya asili na ardhi yao kutumiwa kwa matumizi yasiyokuwa ya umma pamoja na kulipwa fidia ndogo kinyume na makubaliano yao na Serikali, bado yanaendelea kulalamikiwa na wananchi hao siku hadi siku.

(a) Je, Serikali ina ufumbuzi upi wa suala hilo ili kuleta haki kwa wananchi wake.

(b) Kwa kuwa mashamba yaliyokuwa ya wananchi wa kawaida na kuchukuliwa na Serikali kwa ajili ya kilimo cha mpira ya Maziwani (jimbo la Pandani) na Finya (jimbo la Gando) kwa sasa amepewa mtu binafsi asiye mmiliki wa asili, Je, Serikali imeingiza kiasi gani cha fedha kwa miaka mitano iliyopita (2017-2022).

(c) Je, kwa sasa mashamba hayo ya Maziwani (jimbo la Pandani) na Finya (jimbo la Gando) yanatumika kwa shughuli gani.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

146. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika jitihada za Serikali za kuuinua uchumi wa nchi ni kuwasaidia wajasiriamali mbali mbali wa ndani, ikiwa ni pamoja na kununua bidhaa zao wanazozizalisha nchini. Hata hivyo, juhudi hizi bado zinahitajika kwa watengezaji wa samani mbali mbali zinazotumika maofisini.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inazielekeza Wizara na taasisi za Serikali kutumia samani zinazotengenezwa nchini.

(b) Je, kwa mwaka 2021/2022, ni taasisi ngapi za Serikali zimenunua samani zao kupitia watengezaji wa ndani.

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuzitaka taasisi zake kutumia samani zinazotengenezwa nchini.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

191. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo jema sana kuwa Zanzibar kwa sasa ina uwezo wa kusajili meli kupitia Zanzibar Maritime Authority (ZMA).

(a) Je, kwa kipindi cha 2020-2023, ZMA imesajili meli ngapi na zenye sifa gani.

(b) Je, kupitia meli hizo ni mabaharia wangapi wazawa wameweza kuajiriwa na kwa mikataba ya aina gani.

Wizara ya Afya:

235. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali inastahili pongezi kwa kufikiria kuwa na mfumo bora wa afya nchini. Hata hivyo, bado jitihada za maneno hazijaendana na jitihada za vitendo vya Serikali katika kufikia mfumo bora uliokusudiwa.

(a) Je, Serikali haioni ulazima wa kuanzisha idara maalum itakayohusika na matatizo ya msongo wa mawazo ambayo itafanya ushauri nasaha (counselling) kwa wafanyakazi wa Serikali, makampuni binafsi na kwa kila mwananchi ambaye atahitaji huduma hiyo.

(b) Je, Serikali inatumia bajeti na jitihada kiasi gani katika kupunguza uambukizwaji na uzukaji wa maradhi na kiasi gani katika matibabu na dawa.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuanzisha Hospitali za kujifunzia (Teaching Hospitals) katika vyuo na taasisi za afya Zanzibar.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

170. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika bahati tuliyoipata hapa Zanzibar ni kuwa sehemu ya chimbuko halisi la lugha ya Kiswahili fasaha ambacho kinazungumzwa nchini mwetu. Lakini pia tumebahatika kuwa na Makao Makuu ya lugha ya Kiswahili Afrika ya Mashariki.

Je, kwa kiasi gani walimu wetu na wataalamu mbali mbali waliobobea kwenye lugha ya Kiswahili wananufaika na fursa na uwepo wa Makao Makuu ya Kiswahili Afrika Mashariki yaliyopo hapa Zanzibar.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo</u>:**

216. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali imejitahidi kwa miaka mingi kuhakikisha kwamba nchi yetu ina mabibi na mabwana shamba wa kutosha kwa sababu kilimo bado kinachukua nafasi kubwa katika mgawanyo wa shughuli za uchumi wa watu wa Zanzibar. Hata hivyo, wataalamu hawa wamekuwa hawapewi kipambele kinachostahiki na kukosa matunzo.

(a) Je, ni kwa nini mabibi shamba na mabwana shamba walio wengi hawapewi fedha zao za likizo.

(b) Je, ni kwa nini wengi wao wanakosa haki zao za msingi kwa mujibu wa utumishi wa umma.

(c) Je, kama Serikali haijawalipa watumishi hao haki zao za msingi, kwa nini haiziondoi haki hizo kwa taasisi zote ili kuleta usawa na kutowabagua watumishi wake.

226. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Pamoja na jitihada za Serikali za kuzipa kipaumbele shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi kwa mchango wao wa kuendesha maisha ya watu wetu kwa asilimia kubwa, bado jitihada, mikakati na mipango ya kuboresha shughuli hizo inahitajika zaidi.

(a) Je, kwa nini kuna malalamiko ya kukosekana haki na

usawa katika kuhakikisha ugawaji na umilikishaji wa ardhi kwa shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi kwa Wazanzibari wenye sifa.

(b) Je, ni ipi tathmini ya Serikali kuhusiana na mafunzo ya mbinu bora za kilimo, ufugaji na uvuvi, zana na masoko ya bei nzuri za bidhaa kwa wakulima wadogo wadogo.

(c) Kwa vile mpango wa kuwapatia mikopo nafuu kupitia fedha za Uviko 19 umefeli na wananchi wengi kuvunjika moyo, hasa wakulima wadogo wadogo, Je, Serikali haioni ulazima wa kuanzisha taasisi madhubuti za kifedha (mfano Benki ya Wakulima) zitakazorahisisha huduma za kifedha kwa wakulima, wafugaji na wavuvi.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

163. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na majukumu mengine, ina wajibu wa kuutangaza utalii wetu duniani kote, jukumu ambalo linaweza kutekelezwa vyema na vitengo mbali mbali vilivyomo katika Wizara hii.

Je, Wizara yako ina mkakati gani wa kuviboresha vitengo vya ‘Statistics’, ‘Promotion’ pamoja na kitengo cha Utalii wa Ndani (Domestic Tourism Unit) katika kuitangaza na kuiendeleza vyema Sekta ya Utalii.

**Zanzibar,**
**14 Juni, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>**